**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI)**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**

# TAARIFA YA MFUMO WA UKUSANYAJI MAPATO (LGRCIS)

**TAREHE: 31/07/2017**

## 1. UTANGULIZI

Mfumo wa Mapato [*Local Government Revenue Collection and Information System* (LGRCIS)] ulianza kutumika rasmi katika Halmashuri ya Wilaya ya Mpwapwa tarehe 07/03/2016 baada ya watumiaji kupatiwa mafunzo ya utumiaji wa mfumo huu tarehe 04/03/2016 na 05/03/2016.

Pia mfumo wa Mapato (LGRCIS) umeunganishwa na mashine za kukusanyia mapato ***Point Of Sales*** (**POS**) 28 za Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kati ya hizo 13 ni POS zenye muunganiko wa **vichapishi na mashine** ambazo zilianza kutumika tangu tarehe 11/04/2016. Pia kuna POS zingine 15 ambazo ni **Simu** zenye vichapishi pembeni (hazijaunganishwa na vichapishi) na zilianza kutumika kuanzia tarehe 28/11/2016.

Vile vile Mfumo huu *LGRCIS* umeunganishwa na mfumo wa benki ya *National Microfinance Bank* (NMB) unaojulikana kama *Cash Collection System* **(CCS)**. CCS ni mfumo unaomuwezesha mteja/mlipa bili kufanya malipo, kuangalia bili na kuhakiki malipo aliyolipa kwa kutumia SIMU yake ya kiganjani iliyounganishwa na huduma ya **NMB mobile**. Huduma hizi atazipata kwa kuingiza namba ya malipo (**ID: Identification Number)** aliyopewa wakati anasajiliwa kwenye mfumo wa mapato (LGRCIS).

## 2. MAFANIKIO YA KUTUMIA MFUMO WA MAPATO (LGRCIS) NA MASHINE ZA KUKUSANYIA MAPATO (POS).

Kwa ujumla mafanikio ni makubwa tangu matumizi ya mfumo wa mapato (**LGRCIS**) na mashine za kukusanyia mapato (**POS**) kuanza kutumika, hasa katika ongezeko la mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

Kabla ya kuanza kutumia POS 12 toka LIC, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Machi 2016 mapato katika kata 12 yalikuwa **Tsh 25,009,600.00/=** *(Rejea kiambatanisho 'A')*. Vile vile baada ya kutumia POS 12 toka LIC (Local Investment Climate Project) katika kata hizo 12 kwa kipindi cha kuanzia Aprili 2016 hadi Juni 2017 mapato yameongezeka na kuwa **Tsh 387,855,550.00/=** *(Rejea kiambatanisho 'B').*

## 3. FAIDA YA MFUMO WA MAPATO (LGRCIS)

i. Kuwezesha kutoa taarifa sahihi na haraka za kifedha za ukusanyaji wa mapato.
ii. Kutoa risiti na nyaraka mbalimbali za mapato zinapohitajika.
iii. Kufuatilia na kuangalia mapato yaliyokusanywa kwa kutumia POS zilizogawanywa kwa watendaji.
iv. Kuthibiti au kupunguza makosa yaliyojitokeza katika ukusanyaji wa kawaida kwa kutumia vitabu.
v. Kuwawezesha walipa bili kulipa na kuangalia bili zao za huduma mbalimbali kama vile leseni, kwa kutumia simu ya kiganjani iliyounganishwa na NMB mobile kwa kuwa LGRCIS imeunganishwa na CCS.
vi. Kutunza kumbukumbu za mapato na taarifa za walipa bili.
vii. Kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

## 4. MCHANGO WA LIC (LOCAL INVESTMENT CLIMATE PROJECT) KATIKA MFUMO WA MAPATO WILAYANI MPWAPWA.

Kwa ujumla LIC (Local Investment Climate Project) ni mfadhili mkubwa katika mfumo mzima wa ukusanyaji mapato wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa. Vifaa vifuatavyo vilifadhiliwa na LIC katika vipindi tofauti tofauti.

| Na | Kifaa | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Kompyuta za mezani (Desktop) | 7 |
| 2. | Epson printer | 2 |
| 3. | HP Laserjet enterprise M604 | 2 |
| 4. | Barcode reader | 2 |
| 5. | Solar Power bank | 5 |
| 6. | POS (Complete with printers) | 12 |

Vile vile LIC imetuunganisha na kampuni ya Dayone Softcom Technologies ambao ni watengenezaji wa Mfumo wa Mapato (LGRCIS) ili kuweza kuuliza changamoto zozote za mfumo wa mapato (LGRCIS) na POS kwa kupiga simu au barua pepe na kupata msaada bure bila malipo yoyote.

Pia LIC ilifadhili mradi wa kufunga LAN (Local Area Network) katika Jengo la Biashara (One Stop Business Center) ambapo kwa sasa ofisi zote katika jengo hilo zina network na mfumo wa mapato unapatikana na unafanyakazi vizuri.

## 5. MCHANGO WA HALMASHAURI KATIKA MFUMO WA MAPATO (LGRCIS)

- Kugharimia mafunzo kwa maafisa wanaotumia mfumo wa mapato.
- Kuchangia nguvukazi katika kukusanya mapato (Kuunda timu ya mapato).
- Kusimamia na kuhakikisha mapato yanakusanywa kikamilifu kwa kutembelea vituo vya ukusanyaji mapato.
- Kununua risiti za POS (thermal ticket rolls), Epson LQ 590 printers (Computer Generated Receipts) na rimu kwa ajili ya laser jet Enterprise M604 printer ili kutengeneza ankara za wateja.
- Kununua wino kwa ajili ya printer zote yaani Epson LQ 590 printers na laser jet Enterprise M604 printer.
- Kutoa elimu na kuwashawi wafanyabiashara kupitia Baraza la Biashara La Wilaya ili waweze kulipa ankara zao kwa wakati na kuwapa utaratibu wa malipo kwa kutumia kutumia mfumo.
- Kugharimia matangazo kwa njia mbalimbali ya kuhamasisha walipa ushuru na tozo mbalimbali waweze kulipa kwa wakati.

6. **VYANZO VYA MAPATO KATIKA MFUMO WA MAPATO (LGRCIS)**

Vyanzo vya mapato vinavyokusanywa katika mfumo huu wa mapato ni kama vifuatavyo:- (i). Kodi ya huduma (ii). Kodi ya hoteli (iii). Leseni ya biashara (iv). Kodi ya mabango (v). Kodi ya majengo (vi). kodi ya uuzaji wa viwanja (vii). Kodi ya ardhi (viii). Leseni ya vileo (ix) Tozo nyinginezo.

7. **Mikakati ya Halmashauri ya Mpwapwa katika kuongeza POS.**

Halmashuri ya Mpwapwa ina mikakati thabiti ya kuhakikisha kuwa ifikapo Juni mwaka 2017/2018 kila chanzo kitakusanywa kwa POS na kila kijiji kitakuwa na POS moja.

Ifuatayo ni mikakati ya Halmashauri katika kuhakikisha POS zinaongezwa:-

*i.* Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imeshaagiza POS 27 ambazo msambasaji (Dayone Softcom Technologies) alisema kuanzia wiki ya pili ya mwezi Agosti zitakuwa tayari kwa kuwa alishatumiwa LPO (Local Purchasing Order). *(Rejea kitabu cha LPO Na: 0235).*

ii. Pia dokezo la kununua POS 5 limeandaliwa ambapo tunasuburi mfumo wa Matumizi (Epicor) uanze kufanyakazi ili tufanye manunuzi ya POS hizo.

*iii.* Vile vile katika Mpango wa bajeti kwa mwaka 2017/2018 *(Medium Term Plan and Budget for the Financial Year 2017/2018)* Halmashauri *i*metenga Tsh 70,000,000/= ambazo zitawezesha kununua POS 100 za simu na printer. *(Rejea kitabu cha bajeti: Mpango na Matumizi ya Kati kwa mwaka 2017/2018 ukurasa 224).*

**Hivyo kwa mikakati hii ni matumaini yetu mpaka kufikia mwezi Agosti mwishoni tunatarajia kuwa na jumla ya POS 60 na kufikia mwaka Juni 2018 tutakuwa na jumla ya POS 160 ambapo kila chanzo kitakusanywa kwa POS.**

8. **CHANGAMOTO ZA MFUMO**

- Maeneo mengi yanayotumia POS kuwa na tatizo la mtandao na kukwamisha zoezi la ufuatiliaji wa miamala ya papo kwa papo iliyofanywa kwa POS ili kujua kama POS inafanyakazi kwa muda muafaka.
- Kutopata msaada wa haraka kutoka kwa maafisa TEHAMA wa OR – TAMISEMI linapotokea tatizo katika mfumo ambalo linahitaji utatuzi wa haraka.

## 9. UTATUZI WA CHANGAMOTO

- Maafisa Tehama kutoa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mfumo.
- Kutoa maelekezo na matengenezo ya mashine za kukusanyia mapato (POS) kwa watumiaji mahali pa kazi.
- Kufuatilia ukusanyaji wamapato katika minada ili kudhibiti udanganyifu wowote utakaojitokeza na kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato hayo.

Naomba kuwasilisha.